

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

Simu: +25526-230081
Nukushi: +25526-2321170
Barua pepe: km@habari.go.tz
Tovuti: www.habari.go.tz



S. L. P. 25,
Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Habari,
40481 Dodoma.

TAARIFA KWA UMMA

SALAMU ZA POLE

Dodoma – Desemba 15, 2020

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) amepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha Msanii mkongwe wa tasnia ya filamu Mohamed Fungafunga maarufu kama Mzee Jengua, ambaye alifariki, Desemba 15, 2020 Mkuranga Mkoa wa Pwani.

“Hili ni pigo kwa wadau wa tasnia ya Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini, tutamkumbuka kwa kazi yake ya kuburudisha na kuelimisha umma kupitia filamu zake, na unapotaja jina la Jengua unakuwa umetaja jina la moja ya waasisi wa tansia ya filamu nchini waliyovutia vijana wengi kuingia katika uigizaji” alisema Mhe. Bashungwa.

Mzee Jengua atakumbukwa kwa umaarufu wake katika michezo ya runinga kama Kidedea, Kitimtimu na Kizazaa, iliyokuwa ukirushwa na kituo cha televisheni ya ITV, Filamu ya Mke Mwema, Foolish Age na Tamthilia yake ya mwisho ya Tasma pamoja na michezo mingine.

Mhe. Bashungwa ametoa pole kwa Familia, Ndugu, Jamaa, Marafiki, Wasanii, Chama cha Uigizaji Dar es Salaam pamoja na wadau wote wa tasnia ya filamu. Pia anawaomba wote kwa Mwenyezi Mungu, wapate nguvu na moyo wa ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu.

Imetolewa na

Eleuteri E. Mangi
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

